

Ripoti ya elimu ya lugha ya kiutendaji kwa ajili ya utafiti wa eneo wakati 2007

- Kiswahili, chuo kikuu cha Nairobi, Kenya, 7 Feb. 2008 - 31 Mar. 2008 -

Year of Enrollment: 2005

Graduate School of Asian and African Areas Studies

Year in Doctoral course: third grade

Mayuko Inoue

Mafunzo yangu

Kiswahili ni lugha inayozungumzwa katika Afrika mashariki, yaani Tanzania, Kenya na Uganda. Maneno ya Kiswahili mengi yametokea lugha za Kiarabu na Kibantu. Kiswahili kilizaliwa pwani ya Afrika mashariki panapoitwa "SWAHILI" yaani Zanzibar, Kilwa, Mombasa na kadhalika. Mimi ninafanya utafiti wa mambo ya utalii, hasa hasa wachoraji wa utalii wa Zanzibar. Utafiti wangu unahitaji kuzungumza Kiswahili. Kwa sababu watu wanaoishi Zanzibar wanazungumza Kiswahili kizuri. Vilevile wachoraji wa Zanzibar waliotokea bara pia wanaongea Kiswahili sanifu. Kwa hiyo natamani kujifunza Kiswahili sanifu zaidi.

Mwaka elfu mbili na nane, mwezi wa pili, nilijiunga shule ya lugha inayoitwa the Anglican Church of Kenya katika Nairobi, kwa ajili ya kujifunza Kiswahili hasa hasa sarufi, lugha ya heshima na methali. Kwa sababu Kiswahili kina maneno mengi yenye maana moja. Mfano "naenda msalani," "naenda kujisaidia," "naenda maliwato," "naenda chooni." Haya yote yana maana moja. Nafikiri nikijua sarufi vizuri na lugha za adabu vizuri na methali nyingi nitaweza kufaamiana na watu zaidi.

Katika shule, kwanza nilijifunza sarufi kwa mfano kutoka ngeli ya A-WA mpaka ngeli ya KU-KU, na viashiria vya mbali, viashiria vya karibu, na viashiria vya mbali kidogo, sifa za kumiliki, sifa za kuwepo mahali na kadhalika. Nilitumia kitabu cha shule ya msingi darasa la tatu kwa kujifunza sarufi. Kitabu hiki kina mazoezi ya vitendawili pia. Vitendawili ni michezo ya watoto, inayofanana na michezo ya kijapani NAZO-NAZO. Mtoto mmoja akiuliza swali, mtoto mwingine anajibu.

Baada ya kujifunza sarufi, nilijifunza maneno ya heshima kwa mfano nikitaka kumwambia mtu "nataka kwenda chooni," nitamwambia hivi "naende msalani," au "naenda uani." Maneno haya ni lugha ya heshima. Kama mtu akifariki, kusema "amekufa" si vizuri. Ni vyema useme "ameaga dunia" au "amekata kauli." Hizi ni lugha ya adabu. Watu wanaozungumza Kiswahili, wanapenda kutumia maneno ya heshima.

Methali zina maana nyingi zaidi. Kwa mfano mtu akisema "ashindanaye na ndovu chooni hupasuka msamba" maana yake ni "usishindane na mwingine, fanya kwa uwezo wako tu." Kwa sababu methali hii inasema kwamba binadamu hawezi kunya mavi makubwa kama ndovu, bali binadamu hunya mavi yake kama kawaida tu. Kiswahili kina methali nyingi kama hivyo.

Nimejifunza Kiswahili shuleni mpaka mwezi wa tatu mwishoni, lakini bado sijajua kiundani zaidi. Napenda kuendelea kusoma Kiswahili kwa bidii.



Pamoja na mwalimu



Katika darasa



Elimi ni raha